1.0 UTANGULIZI

- Uvumbuzi wa Teknolojia ya matumizi ya DNA (Chembe chembe asili za urithi au Vinasaba) umeonekana kuwa na faida sana katika ulimwengu huu wa Sayansi na Teknolojia inayokuwa kwa haraka na uwezo wa utafiti wa tiba.
- Pamoja na tiba, matokeo ya DNA hutumika katika kutoa haki kisheria.
- DNA hubeba taarifa muhimu za urithi wa binadamu kwa mfano; magonjwa tabia na maumbile.
- Taarifa hizi zinaweza kutumika vibaya na waajiri, watu wa bima na hata katika masomo.
- Kwa sababu hizi ilionekana kuna umuhimu wa kuwa na sheria itakayosimamia matumizi ya Teknolojia hii ya Vinasaba vya Binadamu.

2.0 CHIMBUKO

- Kwa muda wa miaka mingi Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kama ilivyokuwa kwenye Maabara nyingine duniani kote, ilikuwa ikitumia "*ABO Blood Grouping Method*" kwa kumtambua na kumtofautisha binadamu.
- Kutokana na ukweli kuwa 40% ya binadamu wote duniani wana damu group "O" njia hii ya utambuzi iliambatana na ushahidi mwingine mwingi wa macho.
- Njia hii ya utambuzi ilikuwa haitoshelezi kwa vile haimtambui na kumtofautisha binadamu moja kwa moja.

3.0 UMUHIMU WA SHERIA YA VINASABA

- Kuboresha huduma ya Teknolojia hii katika nyanja za kinga na tiba.
- Kulinda athari zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi holela ya teknolojia hii.
- Kuweka taratibu za ukusanyaji, ufungashaji, usafirishaji, upokeaji, utunzaji, utoaji wa matokeo ya uchunguzi na uteketezaji wa sampuli za DNA ya Binadamu
- Kuainisha maafisa waidhiniwa kukusanya, kuchambua na kudhibiti sampuli za DNA ya Binadamu
- Kuweka utaratibu wa utunzaji na utoaji wa matokeo ya sampuli za DNA ya Binadamu.
- Kukusanya na kutunza taarifa mbalimbali za wahalifu kwa matumizi va vyombo husika.

4.0 SHERIA YA VINASABA

- Sheria hii imepitishwa na Bunge Mwezi Aprili, 2009; na kutiwa saini na Mh.Rais Mei, 2009.
- Sheria inajulikana kama *The Human DNA Regulation Act, No.8 of 2009*
- Imegawanyika katika sehemu kuu Kumi na Moja (11)
- **Sehemu ya Kwanza na ya Pili;** zinaongelea jina, wapi sheria hii itatumika na taratibu za kiutawala, kama vile:
- Inamtambua Mkemia Mkuu wa Serikali kuwa ndiye Mdhibiti Mkuu wa Matumizi ya Teknolojia hii ya Uchunguzi wa Vinasaba vya Binadamu.
- **Sehemu ya tatu** inaainisha taratibu za kuanzishwa, kusajili na kutoa leseni, pamoja na ukaguzi wa maabara za Vinasaba vya Binadamu.
- **Sehemu ya nne** inaainisha taratibu za uchukuaji, uhifadhi, usafirishaji na uchunguzi wa sampuli,
- **Sehemu ya tano** inaainisha taratibu za kufanya tafiti mbalimbali, kama za magonjwa na tiba, bila kudhalilisha utu wa mwenye sampuli (Sample Source)
- **Sehemu ya sita** inazungumzia haki za kina mama wajawazito na mimba zinazotungwa nje ya tumbo la uzazi,
- **Sehemu ya saba** inaweka bayana haki za watu wasioweza kujisimamia wenyewe kama vile; watoto, walemavu, wagonjwa.

- **Sehemu ya nane** inaainisha taratibu za kufuata wakati wakutoa taarifa za matokeo za aliyetoa sampuli ya vinasaba na jinsi ya kuteketeza sampuli iliyobaki / isiyotumika tena.
- **Sehemu ya tisa** inaongelea fedha zitakazohitajika kutekeleza sheria hii, zitakavyokusanywa na jinsi zitakavyo tumika,
- **Sehemu ya kumi** inaongelea makosa na adhabu zake,
- **Sehemu ya kumi na moja** inaainisha utaratibu wakutengeneza Kanuni , Kushitaki, kukata rufaa.

5.0 UANZISHWAJI WA MAAABARA TEULE ZA VINASABA

- Kufuatana na sera ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ya kupeleka huduma za afya karibu na jamii, Sheria hii katika Kifungu cha 17 (1) inaruhusu mtu yeyote mwenye utaalamu husika kufungua Maabara ya Vinasaba.
- Maabara za hospitali pia zinaweza kutenga chumba/vyumba kwa ajili ya huduma ya uchukuaji na uchunguzi wa vinasaba

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

Mkemia Mkuu wa Serikali
Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali
Luthuli/ Barack Obama Drive
S.L.P. 164
Dar Es Salaam, Tanzania
Simu: + 255 22 2113383/4
Nukushi: +255 22 2113320
Baruapepe: cgc@gcla.go.tz, gcla@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Mashariki
Luthuli/Barack Obama Drive
S.L.P. 164
Dar Es Salaam, Tanzania
Simu: + 255 22 2113383/4
Nukushi: +255 22 2113320
Baruapepe: gcla.east@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Ziwa,
Eneo la Hospitali ya Sekou Toure/Isamilo
S.L.P. 502,
Mwanza, Tanzania.
Simu: +255 28 2500279
Baruapepe: gcla.lake@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Kaskazini
Kituo cha Afya Themi
S.L.P. 2095
Arusha, Tanzania.
Simu: +255 27 2506394
Nukushi: +255 27 2549026
Baruapepe: gcla.north@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini
Eneo la Hospitali ya Mkoa wa Mbeya
New Forest Area
S.L.P. 2875
Mbeya ,Tanzania.
Simu: +255 25 2502311
Nukushi: +25525 250 312
Barua pepe: gcla.southern@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Kusini
Ushirika House
Barabara ya TANU
S.L.P. 1414
Mtwara,Tanzania.
Simu: +255 23 233 4760
Nukushi: +255 23 233 4761
Barua pepe: gcla.south@gcla.go.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

ISO 9001:2008
ISO 17025:2005

IDARA YA SAYANSI JINAI NA HUDUMA ZA VINASABA

IJUE SHERIA YA VINASABA VYA BINADAMU